# MASS PROGRAM



Greetings in the name of our Lord Jesus Christ:

My dear brothers and sisters in Christ, I wish to take this opportunity to welcome you all to this year's KCCA 9th Annual convention and Swahili mass. Special thanks to Rt. Reverend Joseph Obanyi Sagwe, Bishop of Kakamega Diocese Kenya, who has humbly accepted to be our main celebrant. It is my sincere hope you are all doing fine and for those of you who have been affected by the COVID-19 Pandemic in any way or shape, be assured that we are all in this together so please let's pray for each other.

In the past eight years, the Kenya Catholic Community in America organization has been able to organize and hold Annual Cultural Gatherings that culminate with a Swahili mass. These events have always been excellent and have brought Kenyan Catholics and friends from across the country together to enrich their spirituality from the retreats and Swahili masses. The African cultural events have been a source of joy and give attendees a home feeling experience.

My dear brethren I am excited that this year's event, that was originally scheduled to be held in Brooklyn Park, Minnesota, is now virtual and though we will miss the physical gathering experience, we will still get and strengthen our spirituality as we praise the Lord from our stations in the world…connected through zoom.

For the last nine years that KCCA has been in operation, we have seen tremendous spiritual growth in our communities and many of our brothers and sisters who had strayed from Catholicism are coming back to church. We encourage you all to keep coming and attending our events and to be part and parcel of the evangelization efforts. Our cultural roots are strong, let's not discard them, instead as we assimilate into the American culture let's also influence it with our beautiful cultural heritage. Swahili mass being a big plus.

Lastly, I want to extend my sincere thanks to KCCA leaders who have devoted their time organizing this event, the Kakamega group and all those who volunteered to participate in the event. A huge thank you too, to all convention guest speakers. God bless you abundantly.

Sincerely yours in Christ.

George N Marucha MBA CMA
KCCA: Chairman
www.kcca2012.org
kenyacatholiccommunityamerica@gmail.com

# ENTRANCE SONG/KUIINGIA (KENYA)
# TWENDENI TUINGIE KWAKE

Kiitikio:Twendeni tuingie kwake,
na nyimbo nzuri za shangwe(x2)

1. Dunia nzima imshangilie Bwana, kwa furaha tumtumikie wote, tumwendee na nyimbo za shangwe
2. Mjue Bwana wetu ni Mungu, ametufanya na tuko watu wake, sisi kondoo wa malisho yake
3. Ingieni mlangoni kwa kumsifu, nyumbani kwake tumtolee heshima, tutukuze jina lake kubwa mno
4. Kwa kweli Mungu ni mwema sana, na huruma yake ni ya milele,uaminifu wake kwa vizazi vyote
5. Utukufu kwa Baba Mwenyezi, na kwa mwana mwokozi wetu, na kwa Roho Mtakatifu ndani mwetu

# OPENNING PRAYER: BISHOP OBANYI

# UTUHURUMIE/LORD HAVE MERCY (CA)
# MISA DENNIS

1. Bwana, Bwana tuhurumie –
   Ee Bwana tuhurumie ×2
   Bwaaaana tuhurumie –
   Ee Bwana tuhurumie

2. Kristu, Kristu tuhurumie –
   Ee Kristu tuhurumie ×2
   Kriiiistu tuhurumie –
   Ee Kristu tuhurumie

3. Bwana, Bwana tuhurumie –
   Ee Bwana tuhurumie ×2
   Bwaaaana tuhurumie –
   Ee Bwana tuhurumie

# UTUKUFU JUU KWA MUNGU/GLORY TO GOD (CA) SUBUKIA

{ Utukufu juu kwa Mungu, na amani duniani,
kwao watu wenye mapenzi,
watu wenye mapenzi mema } ×2

1. Tunakusifu tunakuheshimu, twakuabudu tunakutukuza
   Twakushukuru kwa ajili yako, ya utukufu wako mkuu.

2. Ee Mungu baba ndiwe, Mfalme wa Mbinguni baba mwenyezi.
   Ee Yesu Kristu mwana wa pekee, mwanakondoo mwana wa Baba

3. Uondoaye dhambi za watu tuhurumie tusikilize,
   Tuhurumie mwenye rehema maombi yetu uyapokee.

4. Uketiye kuume kwake, Mungu baba tuhurumie.
   Kwa kuwa ndiwe pekee yako, Pekee yako Mtakatifu.

5. Pamoja naye roho Mtakatifu, katika utukufu wake
   Anayeishi na kutawala, milele yote Amina.

# BEFORE READING (CA)
# IENDE MBELE INJILI OH

1. Iende wapi Injili oh -Iende mbele
Iende wapi injili ya Yesu -iende mbele

Chorus:
{Ndiyo maana -Ndiyo maana tunasema iende mbele} ×2

2. Ya bariki injili oh . . .
3. Inaponya injili oh . . .
4. Inakata injili oh . . .
5. Moto moto injili oh . . .

## First Reading: Sr. Mumbi, Chicago

Sikukuu ya Kupalizwa Bikira Maria Mbinguni

# Somo la 1
# Ufu 11:19, 12:1-6, 10
# SOMO KUTOKA UFUNUO WA YOHANA

Hekalu la Mungu lililoko mbinguni likafunguliwa, na sanduku la agano lake likaonekana ndani ya hekalu lake. Kukawa na umeme, na sauti, na radi, na tetemeko la nchi, na mnua ya mawe nyingi sana. Na ishara kuu ilionekana mbinguni; mwanamke aliyevikwa jua, na mwezi ulikuwa chini ya miguu yake, na juu ya kichwa chake taji ya nyota kumi na mbili.

Naye alikuwa ana mimba, akilia, hali ana utungu na kuumwa katika kuzaa. Ikaonekana ishara nyingine mbinguni; na tazama, joka kubwa jekundu, alikuwa na vichwa saba na pembe kumi, na juu ya vichwa vyake vilemba saba. Na mkia wake wakokota theluthi ya nyota za muinguni, na kuziangusha katika nchi.

Na yule joka akasimama mbele ya yule mwanamke aliye tayari kuzaa, ili azaapo, amle mtoto wake. Naye akazaa mtoto mwanamume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma. Na mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi.

Yule mwanamke akakimbilia nyikani, ambapo ana mahali palipotengenezwa na Mungu, ili wamlishe huko muda wa siku elfu na mia mbili na sitini.

Nikasikia sauti kuu mbinguni, ikisema, Sasa kumekuwa wokovu, na nguvu, na ufalme wa Mungu wetu, na mamlaka ya Kristo wake; kwa maana ametupwa chini mshitaki wa ndugu zetu, yeye awashitakiye mbele za Mungu wetu, mchana na usiku.

# Responsorial Psalms: Rose, Boston

## Wimbo wa Katikati
## Zab 45:9-11, 15

Binti za wafalme wamo
Miongoni mwa akina bibi wako wastahiki.
Mkono wako wa kuume amesimama malkia,
Amevaa dhahabu ya Ofiri.

Sikia, binti, utazame, utege sikio lako,
Uwasahau watu wako na nyumba ya baba yako.
**(K) Mkono wako wa kuume amesimama malkia. amevaa dhahabu ya Ofiri.**

Naye mfalme atautamani uzuri wako,
Maana ndiye bwana wako, nawe umsujudie.
Watapelekwa kwa furaha na shangwe,
Na kuingia katika nvumba va mfalme.
**(K) Mkono wako wa kuume amesimama malkia. amevaa dhahabu ya Ofiri.**

# Second Reading: Irene Nyarondia, Kenya

## Somo la 2
## 1Kor 15:20-26
## SOMO KATIKA WARAKA WA KWANZA WA MTUME PAULO KWA WAKORINTHO

Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kiyama ya wafu ililetwa na mtu. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watanuishwa. Lakini kila mmoja mahali pake; limbuko ni Kristo; baadaye walio wake Kristo, atakapokuja. Hapo ndipo mwisho, atakapompa Mungu Baba ufalme wake; atakapobatilisha utawala wote, na mamlaka yote, na nguvu. Maana sharti amiliki yeye, hata awaweke maadui wake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayebatilishwa ni mauti.

**Shangilio**
**Shangilio**
Aleluya, aleluya,
Maria amepalizwa mbinguni majeshi yote ya malaika wanafurahi.
Aleluya.

## GOSPEL ACCLAMATION
## INJILI (KENYA)

Alleluia, alleluia, alleluia x2
Alleluia, alleluia, alleluia
Alleluia, alleluia, alleluia x2

## INJILI/GOSPEL READING
## Lk 1:39-56
## SOMO KATIKA INJILI ILIVYOANDIKWA NA LUKA

Mariamu aliondoka, akaenda hata nchi ya milimani kwa haraka mpaka mji mmoja wa Yuda, akaingia nyumbani kwa Zakaria akamwamkia Elisabeth Ikawa Elisabeti aliposikia kule kuamkia kwake Mariamu, kitoto kichanga kikaruka ndani ya tumbo lake; Elisabeti akajazwa Roho Mtakatifu; akapaza sauti kwa nguvu akasema, Umebarikiwa wewe katika wanawake, naye mzao wa tumbo lako amebarikiwa.

Limenitokeaje neno hili, hata mama wa Bwana wangu anijilie mimi? Maana sauti ya kuamkia kwako ilipoingia masikioni mwangu, kitoto kichanga kikaruka kwa shangwe ndani ya tumbo langu. Naye heri aliyesadiki; kwa maana yatatimizwa aliyoambiwa na Bwana.

Mariamu akasema, Moyo wangu wamwadhimisha Bwana, Na roho yangu imemfurahia Mungu, Mwokozi wangu; Kwa kuwa ameutazama Unyonge wa mjakazi wake. Kwa maana, tazama, tokea sasa Vizazi vyote wataniita mbarikiwa; Kwa kuwa Mwenye nguvu amenitendea makuu, Na jina lake ni takatifu. Na rehema zake hudumu vizazi hata vizazi Kwa hao wanaomcha. Amefanya nguvu kwa mkono wake; Amewatawanya walio na kiburi katika mawazo ya mioyo yao; Amewaangusha wakuu katika viti vyao vya enzi; Na wanyonge amewakweza. Wenye njaa amewashibisha mema Na wenye mali amewaondoa mikono mitupu. Amemsaidia Israeli, mtumishi wake; Ili kukumbuka rehema zake; Kama alivyowaambia baba zetu, Ibrahimu na uzao wake hata milele.

Mariamu akakaa naye kadiri ya miezi mitatu, kisha akarudi kwenda nyumbani kwake.

# HOMILY: BISHOP OBANYI

# NASADIKI/CREED (KENYA)
# KARIOBANGI MASS

1. Nasadiki kwa Mungu moja –
   ninasadiki
   Ndiye Baba wetu mwenyezi –
   Muumba mbingu pia dunia –
   Nasadiki kwa Yesu Kristo –

T/B-(Nasadiki x2 ninasadiki)

2. Mwana wa pekee wa Mungu –
   Mwenye kuzaliwa kwa Baba –
   Akapata mwili kwa Roho –
   kazaliwa naye Bikira –

3. Kasha yeye kasulibiwa –
   Kwa amri ya Ponsyo Pilato –
   Kwa ajili yetu kateswa –
   Akafa na akazikwa –

4. Kafufuka katika wafu –
   Kapaa juu mbinguni –
   Ameketi kuume kwake –
   Mungu Baba yetu Mwenyezi –

5. Ndipo atakapotokea –
   Kuhukumu wazima na wafu –
   Kwake Roho mtakatifu –
   Kwa kanisa la Katoliki –

6. Ushirika wa watakatifu –
   Ondoleo ya dhambi zetu –
   Nangojea ufufuko wa mwili –
   Na uzima wa milele –

**Prayers of the faithful: Stella & Family, Minnesota**

## OFFERTORY/ SADAKA (WORCESTER)

1. Nitakwenda mimi mwenyewe,
   nikatoe sadaka kwa Bwana

   { Aliyeniumba mimi,
   aliyeniumba mimi,
   aliyeniumba mimi
   Mungu wangu,
   Mungu wangu,
   Mungu wangu
   Kwa kuniumba hadi nikapendeza } x2

2. Kaniumba kwa mfano wake, kuliko
   viumbe vingine
   Na sasa nikatoe shukrani

3. Vyote nilivyo navyo ni vyake
   nimrudishie kwa mapendo,
   na sasa nikatoe shukrani

4. Mema mengi amenijalia ya
   mbinguni na duniani
   Na sasa nikatoe shukrani

## MTAKATIFU/ HOLY HOLY (NEW JERSEY)

(Base): Mtakatifu mtakatifu bwana
(Wote): Mtakatifu mtakatifu bwana
mungu wa majeshi ×2

(Base):Mbingu na nchi zimejaa
(Wote): Mbingu na nchi zimejaa utukufu wako ×2
Hosana (Hosana) Hosana, Hosana, Hosana
Hosana, Hosana, Hosana, juu mbinguni (Hosana)

(Base): Mbarikiwa ajayee
(Wote): Mbarikiwa ajae kwa jina la Baba×2
Hosana (Hosana) Hosana, Hosana, Hosana
Hosana, Hosana, Hosana, juu mbinguni (Hosana)

# FUMBO LA IMANI/MYSTERY OF FAITH (KENYA)

Kristu alikufa, Kristu alifufuka Kristu Yesu alikufa, alifufuka, atakuja tena

# GREAT AMEN (KENYA)

Aminaa x4

# OUR FATHER/BABA YETU (KENYA) ALL RECITE

# SIGN OF PEACE/KUPEANA AMANI (KENYA)
# AMANI YA BWANA

1. Amani yako – Bwana

Isambae - Bwana moyoni mwetu daima milele.

2. Furaha yako…
3. Huruma yako…
4. Fadhili zako…
5. Hekima yako…
6. Shukrani zako…
7. Faraja yako…

# LAMB OF GOD/MWANA KONDOO (CA)
# MISA CENTINARY

Ee Mwanakondoo wa Mungu uondoaye dhambi za dunia ee,
Ee mwana tuhurumie
Mwanakondoo wa Mungu ee
Ee mwana tuhurumie
Ee Mwanakondoo wa Mungu . . .
Mwanakondoo wa Mungu ee,
Amani utujalie
Mwenye kuondoa dhambi zetu ee,
Amani utujalie
Utujalie amani ee
A - a –amani, u-utujalie

## ACT OF SPIRITUAL COMMUNION (ENGLISH)

My Jesus,
I believe that You are present in the Most Holy Sacrament.
I love You above all things,
and I desire to receive You into my soul.
Since I cannot at this moment receive You sacramentally,
come at least spiritually into my heart.
I embrace You as if You were already there
and unite myself wholly to You. Never permit me to be separated from You. Amen.

## ACT OF SPIRITUAL COMMUNION (SWAHILI)

Yesu Wangu
Ninaamini kuwa upo katika sakramenti takatifu
Ninakupenda zaidi ya vitu vyote na ninatamani kukupokea ndani ya roho yangu.
Kwa kuwa siwezi kukupokea kwa sakramenti wakati huu,
njoo angalau kiroho ndani ya moyo wangu.
Nakukumbatia kama tayari uko hapo na nijiunge kabisa kwako Usiniruhusu kutengwa na wewe.
Amina

## COMMUNION/KUPOKEA (KANSAS)

{Roho yangu Yesu inakutamani,
njoo kwangu Yesu unipe heri } ×2

1. Nakupenda kwani wewe mwema uniimarishe siku zote
2. Uje kwangu Yesu nakuomba kwani wewe u rafiki mkuu
3. Maumbo ya mkate na divai, umo ndani kweli nasadiki
4. Na uzidi ee Yesu kuwa nami, Unipe uzima wa milele

## THANKSGIVING SONG (WORCESTER)

Jina Maria, ni jina tukufu
Lafurahisha, linatutuliza
Malaika mbinguni wanaliimba, usiku na mchana wanaliimba
(wakisema Ave ave Maria ni jina tukufu jina la Maria)×2

1. Maria mama wa Mungu tuombee,
(tuombee kwa mwanao Yesu Kristu)× 2
2. Jina lako siku zote lapendeza
(wewe uliye mnara wa Daudi)×2
3. Jina lako siku zote lapendeza
(wewe uliye malkia wa Mbinguni)×2
4. Twaliimba jina lako siku zote
(jina Maria linatufurahisha)×2

# ANNOUNCEMENTS
# FINAL BLESSINGS
# EXIT (KENYA) MISA IMEKWISHA

Misa imekwisha - twende na amani kumpenda na kumtumikia Mungu x2

1. Tutangaze injili ya leo … Twende na amani kumpenda na kumtumikia Mungu.Na tutende mema kwa wenzetu….
2. Tuwatunze wasiojiweza …
   Tuwapende maadui zetu …
3. Tuwapende wenzetu wa ndoa Tuwaheshimu wazazi wetu …
4. Tukutane tena Jumapili … Tumtukuze muumba wetu …

# ZOOM INFORMATION

**Topic: KCCA 9TH ANNUAL SWAHILI MASS 2020 AND PRAISE AND WORSHIP**
Please click the link below to join the webinar:
https://us04web.zoom.us/j/78887490425?pwd=S2NKTUtqNDZlOUNDbURtRUdUL0dzUT09
Webinar ID: 788 8749 0425 Passcode: MISA2020
**ZOOM via Telephone**:
Or iPhone one-tap :
US: +13126266799,,78887490425#,,,,,,0#,,85820110# or
+16465588656,,78887490425#,,,,,,0#,,85820110#
Or Telephone:
Dial(for higher quality, dial a number based on your current location):
US: +1 312 626 6799 or +1 646 558 8656 or +1 301 715 8592 or +1 346 248 7799 or +1 720 707 2699 or +1 253 215 8782
Webinar ID: 788 8749 0425
Telephone Passcode: 85820110
International numbers available: https://us04web.zoom.us/u/fwU0GBOVN